



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na HWT/  
09/05/2022

**TANGAZO KWA WANANCHI WOTE**

**Tarehe 12/05/2022**

1. Mtendaji wa kijiji cha Turugeti kimepokea fedha kwa ajili ya **Ukamilishaji wa jengo la OPD zahanati ya Turugeti** fedha kutoka Halmashauri ya wilaya Tarime.
2. Mtendaji wa kijiji cha Turugeti anawatangazia mafundi wote wenye sifa na uwezo wa kufanya kazi ya ufundi walete maombi ya ufundi kwa kazi zifuatazo:

Ukamilishaji wa jengo la OPD  
zahanati ya Turugeti

LGA/067/2021/2022/W/FA/TRGT/01

**SIFA ZA MAFUNDI**

- Mwombaji awe Mtanzania (awe na kitambulisho cha taifa/mpiga Kula
- Awe na barua ya utambulisho kutoka kwa mwenyekiti wa mtaa au **Mtendaji wa Kijiji** ikiwa na picha.
- Mwombaji awe na akaunti Benki
- Mwombaji awe tayari kukosolewa au kushauriwa na mhandisi wa ujenzi
- Mwombaji asiwe amewahi kushitakiwa kwa kosa lolote la kihalifu au kushindwa kutekeleza kazi zinazofanana na hizi.
- Mwombaji awe na uwezo wa kusoma michoro na ramani na kutafasiri (local fundi)
- Mwombaji awe na uzoefu wa kujenga majengo yalioorodheshwa hapo hapo juu
- Fundi atakayefaulu kupata kazi atapewa jaribio la kujenga kwa vitendo.

## MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1. Nyaraka zote zinapatikana katika ofisi ya mganga mfawidhi zahanati ya Turugeti bure , iliyopo Kata ya Bumera Halmashauri ya Wilaya ya Tarime. kuanzia saa 2:00 Asubuhi hadi saa 9:30 Alasiri Siku za kazi. (Jumatatu hadi Ijumaa).
2. Maombi yote yawekwe kwenye bahasha na kufungwa vizuri na kuandikwa juu ya bahasha maneno ya fuatayo:-  
Mtendaji wa Kijiji ,  
S.L.P 16,  
Tarime.

### MFANO

Ukamilishaji wa jengo la OPD zahanati ya Turugeti  
Zabuni Na LGA/067/2021/2022/W/FA/TRGT/01

3. Mwisho wa kurudisha maombi ni tarehe 18/05/2022 saa 4:00 Asubuhi na baadaye zitafunguliwa saa 4:30 asubuhi. Maombi/zabuni zitakazochelewa, za kielektroniki, na zabuni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguaji wa zabuni kwa hali yoyote ile hazitapokelewa wala hazitakubaliwa kwa tathimini.

*Nyamwaga - D. Marwa*  
.....  
Mtendaji wa kijiji  
Kijiji cha Turugeti  
Tarime

VILLAGE EXECUTIVE OFFICER  
TURUGETI - TARIME.  
*Manelouze*  
0766428657